


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz

Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Utumishi,
S.L.P 670,
DODOMA.

DODOMA
08 Juni, 2023

TAARIFA KWA UMMA

**KUKAMILISHWA KWA TARATIBU ZA UTEUZI NA UHAMISHO WA MAKATIBU
TAWALA WA WILAYA NA WAKURUGENZI WATENDAJI WA MAMLAKA ZA
SERIKALI ZA MITAA**

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inapenda kuwajulisha Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Serikali za Mitaa walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, wanatakiwa kuripoti katika vituo vyao vya kazi walivyopangiwa ifikapo tarehe 12 Juni, 2023 wakati taratibu nyingine za kukamilisha teuzi zao zikiendelea.

Taarifa hii inatolewa kufuatia Taarifa kwa Umma iliyotolewa na Mkuu wa Utumishi wa Umma (Katibu Mkuu Kiongozi) tarehe 07 Juni, 2023 ambapo ilielezwa kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya mabadiliko ya Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Serikali za Mitaa ambapo katika mabadiliko hayo, Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi mpya pamoja na kuwahamisha vituo vya kazi baadhi ya Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ofisi inawatakiwa maandalizi mema na kazi njema.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Juma S. Mkomi'.

Juma S. Mkomi
KATIBU MKUU (UTUMISHI)